

Taasisi ya Thirldmill

Beji ya Maombi

Haleluya. Mshukuruni BWANA, liitieni jina lake, Wajulisheni watu matendo yake. Mwimbieni, Mwimbieni kwa zaburi, Zitafakarini ajabu zake zote. Jisifuni kwa jina lake takatifu, Na ufurahi moyo wao wamtafutao BWANA. Mtakeni BWANA na nguvu zake, utafuteni uso wake siku zote.

Zaburi 105:1-4

Katika mambo mengi unayoweza kujifunza ya kweli, wazo la maombi na kujifunza juu yake katika Maandiko hayatakuwa na athari kubwa katika maisha au huduma yako usipofanya kwa vitendo. “Ujuzi na elimu” juu ya maombi pekee hautakuwa na athari kubwa kwako. Ingawa beji hii itakusaidia kukuongoza katika majadiliano juu ya maombi unapojiandaa kuyafanya, kipengele kikuu cha beji hii na mazoezi halisi ya jambo hilo. Omba pamoja na kikundi chako, omba pamoja na mkufunzi wako, omba pamoja na kusanyiko lako, na pia omba peke yako na Mungu.

Vipengele vya Beji¹:

Kumwangukia Mungu, Maombi yetu yanasema nini juu ya mtazamo wa Mungu?
Kujiangukia Sisi, Maombi yetu yanasema nini kutuhusu sisi?
Kuyangukia maombi Yetu, Maombi yetu yanachukua muundo gani, na kwa namna gani yanaweza kuboreshwa?

Mada za Kujadili:

1. Umekuwa na uzoefu gani na maombi? Maombi yako ya wakati huu yakoje?
2. Ni kwa kiasi gani tunamtegemea Mungu? Ni kwa namna gani wazo hili ni la msingi katika maombi?
3. Ni jinsi gani ufafanuzi wa tabia ya Mungu unatusaidia sisi kumtegemea zaidi Mungu tunapomwomba? Toa mifano michache ambayo inatumika katika maombi ya kibiblia.
4. Orodhesha Baraka tano ulizokwisha kupokea kama matokeo ya kifo na kufufuka kwa Kristo. Pia, orodhesha mambo matano unayongoja kupokea kutoka kwa Kristo.
5. Soma Zaburi ya 30 na kuijadili. Ni kwa njia gani maombi yanaweza kuwa njia ya furaha tunapomba?

¹ Mhutasari wa msingi wa beji hii na Majadiliano yamechukuliwa kutoka katika kitabu cha Richard L. Pratt, Jr., *Omba ukiwa umefungua macho yako* (Philipsburg, NJ: Presbyterian na kampuni ya Reformed Publishing, 1987).

6. Ni kwa njia zipi maombi yanaweza kututoa kutoka katika shina la uchoyo? Tunaweza kuzuia maombi ya ubinafsi kwa namna gani?
7. Kama Mungu ni huru na asiyebadilika, kwa nini tunaomba? Je, Mungu hujibu maombi yetu kweli?
8. Uhuru, Upole, unathamani gani katika maombi? Kuna athari gani kama mmoja wetu anasisitiza ubaguzi wa wengine? Ni kwa namna gani athari hizo zinaweza kuzuilika?
9. Ni njia gani tofauti unazoweza kuzitumia kuomba? Eleza faida ya kila moja.
10. Mathayo 6:5-15 ni sala ya Bwana. Isome na kuijadili. Unajifunza nini kuhusu kuomba katika kifungu hiki?
11. Ni vipengele gani vya Sala ya Bwana unaweza kuviingiza katika maombi ya maisha yako?
12. Kuna kusudi gani la msingi kuonesha shukrani katika maombi? Ni mara ngapi tunakosa kuonesha mwelekeo huu katika maombi?
13. Kwanini Lugha ya mwili ina thamani katika maombi? Ni misimamo gani inayofundishwa katika Biblia? Ni kwa namna gani tunaweza kuanza kutumia lugha ya mwili katika maombi?

Mambo ya Kufanya:

1. Kwa kufuata hatua ulizofundishwa na mkufunzi wako, tenga muda binafsi kwa ajili ya kuomba.
2. Kwa kuzingatia mambo mengi yaliyozungumziwa katika beji hii, tumia muda wa maombi pamoja na kikundi chako au marafiki zako.
3. Kwa kufuata hatua ulizofundishwa na mkufunzi wako, ongoza maombi katika kanisa lako la mtaa.

Vigezo vya Beji:

Utatunukiwa Beji hii na tasisi ya Thirldmill kama sehemu ya Cheti cha Misingi baada ya kufuzu vigezo vyote vya Beji vilivyo kwenye **mambo ya kufanya** kwa uaminifu, na **uthabiti**, na kwa kufuata **vipengele vya Beji** na muktadha wa **mada zilizozungumziwa** katika kipindi chote cha kozi.